

## WIZARA YA AFYA, MEANDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO.



### TAARIFA KWA UMMA

Uhakiki wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali umekuwa ukiendelea hapa nchini kuanzia tarehe 21 Agosti, 2017 na ulitarajiwa kukamilika tarehe 4 Septemba, 2017. Uhakiki huu ambao ulifanyika katika Kanda Tano (5) zikiwemo Kanda ya Mashariki/Kusini, Kanda ya Kati, Kanda Kaskazini, Kanda ya Nyanda za Juu Kusini na Kanda ya Ziwa umehusisha NGOs zote nchini. Baada ya kutathmini mwenendo wa uhakiki na kutokana na maombi ya wadau tumeamua kuongeza muda wa uhakiki kuanzia tarehe **5 Septemba, 2017 hadi 20 Septemba, 2017.**

Tunapenda kuwakumbusha wadau kutumia muda huu wa nyongeza vizuri na kwamba hakutakuwa na fursa ya kuongeza muda tena. Ikumbukwe kuwa baada ya tarehe 21 Septemba, 2017 Msajili atahuisha Rejista ya Usajili wa NGOs na Mashirika ambayo yatakuwa hayajahakikiwa yatachukuliwa kuwa yamekufa na hivyo kuondolewa kwenye Rejista ya NGOs. Aidha, mashirika hayo yatatangazwa kwenye magazeti na kuwekwa kwenye Tovuti ya Uratibu wa NGOs na mitandao mbalimbali ya kijamii. Ikumbukwe kuwa wakati wa uhakiki kila shirika linapaswa kuwasilisha Cheti Halisi cha Usajili, Nakala ya Cheti cha Usajili, kujaza fomu ya uhakiki (**NGO-Fomu/UHK/2017**) inayopatikana katika Tovuti ([www.tnnc.go.tz](http://www.tnnc.go.tz)), Stakabadhi za Malipo ya Ada ya mwaka toka kuanzishwa kwa shirika na nakala ya katiba iliyothibitishwa na Msajili wa NGOs (*mashirika yaliyosajiliwa chini ya Sheria ya NGOs tu*) na Mashirika mengine yenye sifa za “NGOs” ambayo yamesajiliwa katika Sheria nyingine yanapaswa kuwasilisha Katiba, Barua kutoka kwa Afisa Maendeleo ya Jamii wa Mkoa, Wilaya au Manispaa ikithibitisha uwepo wa Ofisi ya Shirika. Kadhalika, inasisitizwa kuwa mashirika yote yanayofanya shughuli za NGOs hata kama wamesajiliwa kwenye Sheria nyingine yanapaswa kushiriki kwenye uhakiki huu na watapewa maelekezo stahiki baada ya kuhakikiwa.

A handwritten signature in blue ink, appearing to read 'Katemba'.

M.S. Katemba

**MSAJILI WA MASHIRIKA YASIYO YA KISERIKALI**